

HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE. MAGALULA SAID MAGALULA KATIKA KONGAMANO LA NNE LA VYAMA VYA USHIRIKA MANISPAA YA SUMBAWANGA TAREHE 25 JANUARI, 2016

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,
Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga,
Mrajis Msaidizi wa vyama vya Ushirika Mkoa wa Rukwa
Viongozi wa Taasisi za Umma na Taasisi binafsi,
Viongozi wa Vyama Vya Ushirika,
Waandishi wa Habari,
Wageni waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana mahali hapa siku hii ya leo.

Nichukue fursa hii kuwapongezeni Waandaaji wa Kongamano hili la vyama vya Ushirika Manispaa ya Sumbawanga, ni wazo zuri kuwa na Kongamano hili kwa kuwa ni uwanja mpana wa kujadili mustakabali wa shughuli za ushirika na maendeleo yake ndani ya Mkoa.

Wazo hili lilipofika mezani kwangu nilitoa maelekezo nikiwataka waandaaji waongeze wigo kwa kushirikisha Wadau wengi zaidi kwa kuwa changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya Ushirika zinaelekeana karibia Mkoa mzima, pia kwa ushiriki wa Wadau wengi zaidi, itatoa nafasi ya wengine kujifunza wenzano

wanafanya nini na namna wanavyozikabili changamoto wanazokumbana nazo.

Sekta ya ushirika ni muhimu kwa maendeleo ya Mkoa kutokana na idadi kubwa ya Wananchi wetu kutegemea kilimo kama shughuli kuu ya kiuchumi. Sekta ya ushirika ni muhimu kwa kuwa itasaidia maendeleo ya Mkulima binafsi na Maendeleo ya Mkoa kwa ujumla.

Pamoja na Wananchi wetu kutegemea kilimo zaidi kama shughuli kuu ya kiuchumi lakini zipo fursa mbalimbali katika Sekta nyingine ambazo shughuli za Ushirika zinafanyika na kuleta maendeleo.

Nimejulishwa kuwa kila mwaka mnafanya kongamano mkiwa na malengo ya kujitathmini wapi mlipotoka, mlipo sasa na kupanga mipango madhubuti ya kuhakikisha mnafanikiwa katika utekelezaji wa shughuli zenu za kiushirika ili kufikia malengo mliojiwekea. Malengo haya ni mazuri lakini kuna haja ya kwenda mbali zaidi ya hapo.

Kuna haja katika makongamano kama haya tufahamishane kwa ushahidi wa dhahiri Chama cha Ushirika fulani "kwa mfano" kilikuwa hapa mwaka uliopita na kwa sasa kipo pale na changamoto ya ukosefu wa mikopo imeweza kupatiwa ufumbuzi kwa namna gani au idadi ya mikopo iliyotolewa mwaka uliopita kwa mwaka huu imeongezeka mikopo mingapi kutoka katika taasisi za fedha ukilinganisha na mwaka uliopita, kwa maana nyingine kuwa na idadi ya Vyama vingi zaidi vilivyokopesheka tofauti na idadi ya mwaka jana.

Makongamano haya yasiwe kama sehemu ya kukutana na kufahamiana na mwisho kutawanyika "business as usual" uwepo wa Makongamano haya lazima yaletwe tofauti ndani ya Mkoa. Tofauti ambayo inaonekana bila kutafutwa kwa tochi.

Nimeambiwa kwamba Kongamano la kwanza mlilifanya tarehe 30.09.2012, Kongamano la pili mlilifanya tarehe 22.02.2014. kwa maana nyingine kwa mwaka 2013. Kongamano la tatu mlilifanya tarehe 25.02.2015 na Kongamano la nne ni leo tarehe 25.02.2016. ninapenda kutoa wito makongamano haya yafanyike kwa mtiririko mzuri wa kila mwaka. Muda wa mwaka mmoja ni muda wa kutosha kuweza kufanya utekelezaji wa maazimio yanayofikiwa na kutoa taarifa ya utekelezaji katika kongamano linalofuata.

Mkoa wa Rukwa bado tupo nyuma katika Sekta ya Ushirika, tofauti na Mikoa mingine ambayo Sekta ya Ushirika ina nguvu sana kutokana na Sekta ya Ushirika kuwepo katika maeneo yao kwa muda mrefu. Hata hivyo sisi kama Wadau tunawajibu wa kuikuza Sekta ya Ushirika ndani ya Mkoa ili tufikie viwango walivyofikia wenzetu katika Mikoa mingine.

Hata hivyo kutokana umuhimu wa Sekta hii ya Ushirika nimetoa maelekezo tufanye Kongamano kubwa la Wadau wa Mahindi ndani ya Mkoa, Kongamano hili litahusisha wengi wa Wadau mliopo mahali hapa. Katika Kongamano hilo tutajadiliana namna bora ya kupelekea Mkoa wetu mbele kupitia zao la Mahindi zao ambalo ndiyo utambulisho wetu. Kwa namna moja au nyingine katika Kikao hicho tutapata mwelekeo na sote tutaongea lugha moja.

Kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya tano ni ukusanyaji wa mapato ya ndani hususani kwa Halmashauri zetu ili tuweze kutekeleza miradi ya maendeleo ipasavyo kulingana na mazingira yetu. Hivyo Sekta ya Ushirika ni moja ya taasisi wezeshi kufikia lengo hilo, kwa kutumia mpango au mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani, mfumo huu ni mzuri kwa kuwa unaongeza pato kwa Mkulima na pia Halmashauri kwa maana ya ushuru wa mazao pia mfanyabiashara anapata fursa ya kuuza mazao yake kulingana na bei ya soko kwa wakati anaotaka.

Kama Mkoa tumedhamiria na katika hili tunataka tuongeze mapato kwa kuweka mikakati ya pamoja kwa kuwa karibu na wazalishaji katika maeneo ya shughuli zao, kama ni mkulima shughuli za Afisa ugani ziwe karibu na Mkulima kuanzia uchambuzi wa mbegu bora na kufuata kanuni bora za kilimo na kama ni mfanyabiashara apate huduma nzuri za masoko kwa kuongeza thamani mazao na kwa wanunuzi wa mazao basi kuwepo na maeneo maalumu "magulio" ambapo mfanyabiashara au mnunuzi anakutana na mkulima na kwa kutumia vipimo au mizani waweze kufanya biashara.

Kwa kufanya hivyo itamsaidia mfanyabiashara kununua mazao yake kwa idadi anayoitaka kwa urahisi pia itamsaidia mkulima kuuza mazao yake kwa vipimo sahihi na Halmashauri kupata ushuru stahiki na kuweza kuwa na tawimu za uzalishaji zilizo sahihi.

Ni vema kila mmoja wetu akatambua muelekeo wetu katika masuala ya biashara na mazao ya kilimo ili aweze kushiriki ipasavyo.

Kwenye taarifa yenu mmeleza kuwa Vyama Vya Ushirika wa Mazao (AMCOS) vipo vinne (4) Vimeweza kuuza Mazao kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na kiasi cha jumla ya Tani 3,467 kwa msimu wa mwaka 2013, 2014 na 2015 sawa na shilingi 1,733,500,000. Vyama Vya Ushirika 2 kwa utaratibu wa hiari vimejiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii NSSF na wanachama wake 17 wameshachangia kiasi cha shilingi 4,780,000 katika mfuko huo. Aidha, Chama 1 cha Ushirika kimejiunga na Mfuko wa Bima ya Afya kwa utaratibu wa kuchangia kwa hiari na wanachama 8 wanaendelea kupata huduma ya Bima ya Afya kama watumishi wengine walioko kwenye sekta rasmi wanavyopata huduma hii. Hilo ni jambao zuri na la kuiigwa na Vyama vingine

Mdau wa Maendeleo Bank ya CRDB imeweza kukopesha jumla ya shilingi 1,718,000,000/= kwa vyama vya ushirika vinne (4) na mkopo huo ni wa kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita. Kiasi hicho cha mkopo kinaonesha jinsi gani tunavyotakiwa kufanya kazi kujengea uwezo Vyama vyetu ili viweze kunufaika na fursa ya mikopo kutoka taasisi za fedha . Sehemu nyingine kiwango hicho kinaweza kukopwa na Chama kimoja tu cha Ushirika. Hivyo hilo liwe changamoto ya kuifanyia kazi.

Yapo masuala ambayo Maafisa Ushirika wanao wajibu wa kuhakikisha yanapatiwa ufumbuzi kwa kuwa ndiyo wajibu wao wa kila siku, Masuala ya utoaji elimu wa uundaji wa Vyama Vikuu vya Ushirika, uandaaji wa Hesabu kwa mujibu wa matakwa ya Kisheria, na Kujenga Mitaji ya ndani ya Vyama

Napenda kuhitimisha kwa kutoa msisitizo, tuone uwezekano wa kuhakikisha Kongamano lijalo linakuwa na sura na taswira ya KiMkoa ili kuweza kujengea uwezo sisi kwa sisi na kubadilishana uzoefu.

Fursa ya Kongamano hili itumike vizuri na kuweka maazimio ambayo utekelezaji wake utolewe taarifa katika Kongamano lijalo. Kongamano ni tofauti na maadhimisho, Kongamano linatoa muelekeo na kuweka vipaumbele kwa mwaka husika, na mikakati ya kufikiwa maelengo hayo.

Baada ya kusema hayo sasa napenda kutamka kuwa " Kongamano la Vyama vya Ushirika limefunguliwa rasmi"

Asanteni kwa kunisikiliza.

Magalula S. Magalula

MKUU WA MKOA

RUKWA